# Sera ya Msaada wa Kifedha

BJC Health ("BJC") ingependa kuwasaidia wagonjwa ambao hawana bima ya afya au ambao wanahitaji msaada wa kulipa bili zao za hospitalini. Kama shirika lisilo la faida la huduma za afya, BJC na hospitali zetu wanachama pamoja na mashirika yetu ya huduma za afya wanajali wagonjwa na jamii tunazohudumia kupitia afya bora na huduma za afya zenye ubora.

Wafanyakazi wetu wanaweza kukusaidia:
- Omba bima ya afya kupitia Soko la Afya
- Kuomba msaada wa bima ya Medicaid
- Kubaini endapo unastahiki msaada wa kifedha kutoka BJC

### Msaada wa Kifedha wa BJC
Kabla ya yote, hali yako ya kifedha haitaathiri huduma yako. Wagonjwa wote hupewa heshima na usawa. Wagonjwa ambao wanafikia miongozo fulani ya kipato wanaweza kustahiki msaada wa kifedha wa BJC, ikiwa ni pamoja na gharama zilizopunguzwa za hospitali na mipango ya malipo ya muda mrefu na isiyotozwa riba. Wagonjwa ambao wanastahiki msaada wa kifedha watalipishwa bili kwa kiasi kidogo zaidi ya kile ambacho kwa kawaida hutozwa watu wenye bima inayolipia huduma hiyo. Taarifa kuhusu kiasi kinachotozwa kwa ujumla na jinsi inavyotolewa inapatikana kwa kuwasiliana nasi kupitia taarifa za mawasiliano zilizo chini ya ukurasa huu.

Ikiwa una bima ya afya na una maswali kuhusu bima na kiwango cha manufaa yako, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa bima yako. Wagonjwa wasio na bima watapata punguzo la moja kwa moja la asilimia 40 kwa gharama zinazotozwa na watazingatiwa kwa msaada.
Kwa kutegemea aina ya huduma na kiwango cha msaada wa kifedha, kiasi fulani cha malipo kinaweza kuhitajika. Tunaweza kukupatia chati ya Kipato na Punguzo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ambayo inaonyesha kiasi cha kulipa endapo utaomba.

Idhini ya msaada wa kifedha itatumika kwa miezi 12 tangu tarehe ilipoidhinishwa. Wagonjwa waliohudumiwa katika kipindi hiki wanapaswa kutujulisha kuhusu ziara yao kwa kuwasiliana nasi kupitia taarifa za mawasiliano zilizo chini ya ukurasa huu, ili msaada wa kifedha uweze kutumika. Upekee wa kutofuata vigezo vya kupata msaada wa kifedha unaweza kuzingatiwa kulingana na hali ya mtu.

### Uombaji Msaada wa Kifedha
Unaweza kuomba msaada wa kifedha muda wowote - kabla, wakati au baada ya huduma yako, hadi siku 240 baada ya bili yako ya kwanza. Tutatuma maelezo pamoja na bili yako kuhusu namna ya kuomba msaada. Maombi pia yanapatikana kwa kuomba katika kituo chochote cha BJC na kwenye tovuti zetu za BJC.org au SaintLukesKC.org. Maombi yanahitaji uthibitisho wa kipato kama vile taarifa za malipo ya kodi ya mapato au stakabadhi za malipo ya mshahara. Mifano ya nyaraka ambazo zinaweza kutumika kama uthibitisho wa kipato inaweza kuonekana kwenye fomu ya maombi.

Wagonjwa waliojiandikisha katika Medicaid katika miezi sita iliyopita wanastahiki moja kwa moja msaada wa kifedha kwa huduma za matibabu ambazo hazifadhiliwi na Medicaid. (Utofauti pekee ni kama usajili uliopita wa Medicaid ulitokana na ujauzito. Katika hali hiyo, bado unaweza kuomba kupata Msaada wa Kifedha.)

Zaidi ya hayo, wagonjwa wanaweza kuidhinishwa kupata msaada wa kifedha kwa kutumia mbinu ya kawaida ya uchambuzi ambayo hukadiria hadhi ya kifedha na/au kijamii-kiuchumi ya mgonjwa. Kustahiki aina hii ya msaada hakumaanishi moja kwa moja kuwa mgonjwa atastahiki msaada kwa akaunti za baadaye.

### Ustahiki wa Kimatibabu kwa Msaada wa Kifedha
Hospitali za BJC zitatoa, bila ubaguzi, huduma za matibabu za dharura kwa wagonjwa wote wanaohitaji huduma hizo, bila kujali uwezo wao wa kulipa au kustahiki msaada wa kifedha, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Huduma za Dharura za Matibabu na Uzazi (Emergency Medical Treatment and Active Labor Act, EMTALA).

Msaada wa Kifedha unapatikana tu kwa huduma za dharura na zilizo muhimu kitabibu. Haitumiki kwa taratibu zisizo za lazima kama vile upasuaji wa urembo. Pia hautumiki kwa sehemu ya huduma zako ambazo zimeshalipiwa na mhusika mwingine kama vile kampuni za bima au mpango wa serikali.

Msaada wa kifedha unapatikana kwa wagonjwa wanaoishi Kansas, Missouri, na Illinois, pamoja na wagonjwa wote wanaopata huduma kwenye vituo vya Shirika la Kitaifa la Huduma za Afya (National Health Service Corps,NHSC) bila kujali wanapoishi. Vituo vya NHSC vya BJC HealthCare ni pamoja na Missouri Baptist Sullivan Hospital Bourbon Medical Office, Cuba Medical Office, Steelville Medical Office, na Sullivan Medical Office; na Parkland Health Center Medical Clinic. Vituo vya NHSC vya Saint Luke’s ni pamoja na Allen County Clinic–Iola, Kituo cha Huduma za Familia cha Anderson County, Kliniki ya Huduma za Familia ya Hedrick, Kituo cha Matibabu cha Hedrick, Wakala wa Hedrick OB GYN, Kliniki ya Saint Luke’s Mercer County, Hospitali ya Wright Memorial, na Kundi la Madaktari wa Wright Memorial.

Orodha ya watoa huduma ambao hawajajumuishwa chini ya sera ya msaada wa kifedha ya BJC inapatikana kwa kuwasiliana nasi kupitia taarifa za mawasiliano zilizo chini ya ukurasa huu.

### Miongozo ya Kipato kwa Msaada wa Kifedha
Kiasi cha msaada wa kifedha unaopata unatokana na taarifa za Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho kinachowekwa na serikali ya Marekani kila mwaka. Ili kustahiki kupewa punguzo, kipato cha familia yako ni lazima kisizidi mara tatu zaidi ya Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (asilimia 300). Tunaweza kukupatia chati ya Kipato na Punguzo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ambayo inaonyesha viwango hivi vya kipato endapo utaomba. Zaidi ya kipato chako, punguzo pia litatilia maanani ukubwa wa familia yako. Wagonjwa wenye kipato cha familia kinachozidi $100,000 kwa mwaka hawastahiki msaada wa kifedha wa BJC, bila ya kujali ukubwa wa familia. Wakazi wa Illinois ambao hawana bima wanaopata huduma kwenye hospitali za Alton Memorial, Memorial Hospital huko Belleville na Memorial Hospital huko Shiloh wanaweza kustahiki mapunguzo ya ziada chini ya Sheria ya Punguzo kwa Mgonjwa asiye na Bima Hospitalini ya Illinois(Hospital Uninsured Patient Discount Act).

### Miongozo ya Kipato kwa Matukio ya Majanga
Kunapokuwa na tukio la janga la kimatibabu, wagonjwa ambao kwa kawaida wanaweza wasistahiki kupata Msaada wa Kifedha watapewa msaada. Chini ya hali hizi maalum, wajibu wa malipo ya mgonjwa katika kipindi cha miezi 12 hautazidi Asilimia 20 ya mapato ya familia kwa mwaka.

### Tafadhali Wasiliana Nasi
Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu sera ya msaada wa kifedha ya BJC, sera zinazohusiana, na fomu ya maombi, au kufanya ombi. ili kupokea taarifa iliyoandikwa au mawasiliano kwa njia ya kielektroniki, wasiliana na mwakilishi wa Huduma za Wagonjwa au piga simu kwa:
- BJC HealthCare kupitia namba 314-362-8400 au 855-362-8400
- Saint Luke’s kupitia namba 816-932-5678 au 888-581-9401
- St. Louis Children’s katika CoxHealth kupitia namba 417-815-8846 au 833-345-1395. Taarifa na fomu za maombi pia zinapatikana kwenye BJC.org. au SaintLukesKC.org.

**Tafadhali jisikie huru kuulizia kuhusu msaada wa kifedha. Tuko hapa kukusaidia.**

3259250-02-03-2026